

# Pambazuko

Toleo Namba 028

Jumatatu Januari 23-29, 2023

## Hakimu auawa kwa mawe

Uk. 5



## Harufu ya rushwa Mv Mapinduzi

Uk. 13

## Chadema wapanga 'kupindua meza'

## Wajerumani kurudisha mafuvu 200 waliyopora

Uk. 4

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

## Mhimili wa Pambazuko

**G**AZETI la Pambazuko linandelea kujenga heshima kwa kuwapa wasomaji wake habari ambazo zimefanyiwa kazi kwa kina.

Pambazuko limekuwa gazeti la mfano na rejea mahali pengi tangu kianzishwa kwake mwaka jana na linaendelea kujiimarisha kitaaluma kadri inavyowezekana.

Ni kutokana na imani kutoka kwa wasomaji wake, tumeona ni vyema kuweka kwa umma misingi na imani za waandishi wa habari wa Pambazuko ili kila msomaji atambue kuwa watendaji wa Pambazuko wanasimama katika imani za namna gani.

Watu wengi wameuliza, je, Pambazuko ni gazeti kama magazeti mengine, mbona limekaa tofauti na watendaji wa vyombo vingine vya habari ambavyo vimezoeleka?

Jibu la swali hili ni rahisi kwa maana kwamba waandishi wa habari wa Pambazuko wanasimamia imani 10 ambazo zimekuwa mwongozo wa utendaji wao wa kila siku.

Pamoja na kwamba gazeti hili husambazwa bure kwa njia ya WhasApp, ni chombo ambacho kimesajiliwa na kutambuliwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa pande zote mbili; Tanzania Bara na Zanzibar.

Hivyo, ni chombo cha habari chenye hadhi sawa na magazeti, radio, vituo vya televisheni na vyombo vingine rasmi na vinavyotambulika.

Mhariri Mkuu  
Januari 23, 2023

### Imani 10 za mwandishi wa Pambazuko

1. Kwamba kufikiri na kuamua kwa uwazi, usahihi na kuandika habari kwa kuzingatia miiko ya uandishi wa habari ndiyo msingi wa kazi zangu.

2. Kwamba kamwe sitaandika habari za kutunga, uongo wala uzandiki kwa lengo la kudanganya jamii au kuumiza yeyote.

3. Kwamba nitahakikisha kinachopelekea kwa mhariri ni ukweli, tena ukweli mtupu.

4. Kwamba nitaweza kuitetea – kwa ushahidi, habari ambayo nitaandika hata ikiwa ni mahakamani.

5. Kwamba nitashiriki kuhakikisha matangazo, habari, makala, safu na hata barua za wasomaji zinazingatia miiko ya uandishi wa habari na kamwe hazina lengo lililojificha.

6. Kwamba ubora wa kazi zangu – kupitia Pambazuko, utapimwa kwa uadilifu, uaminifu na usahihi wa kile kinachochapisha.

7. Kwamba, kumcha Mungu ni chanzo cha maarifa na uandishi bora, elimu bora; darasani na chumba cha habari cha Pambazuko, ni sehemu muhimu kujiendeleza kitaaluma.

8. Kwamba sitaogopa kuandika ukweli, hata kama utaumiza baadhi ya watu. Lengo ni kuponya jamii pana.

9. Kwamba rushwa ni adui wa haki, sitatoa wala kupokea na nitaandika wanaojihusisha nayo ili kuokoa jamii.

10. Ninaamini kuwa uandishi bora wa habari siku zote unajali utu, kamwe sitabagua.

3



## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

## **NUKUU**



Lengo la elimu ni kuwaongoza vijana katika mchakato unaowafinyanga kuwa watu wenye silaha ya maarifa, uthabiti wa uamuzi, na tunu za kimaadili, ambao pia unawawezesha kuwa warithi kamili wa mataifa yao na ustaarabu wa kitaifa uliomo~Jacques Maritain, mwanafalsafa wa Marekani aliyehusika pia kuandaa Tamko la Umoja wa Mataifa Kuhusu Haki za Binadamu.

---

## **Mafuvu 200 yaliyoporwa na Ujerumani kurejeshwa Tanzania**

**Na Mwandishi WETU**

**S**ERIKALI ya Ujerumani imejiridhisha kwamba mafuvu zaidi ya 202 ya binadamu yaliyokuwa yakihifadhiwa nchini humo na baadaye kufanyiwa uchunguzi ili kutambua asili yake, ni “mali ya Tanzania”, hivyo kuanza kurejeshwa.

Mafuvu hayo ni miongoni mwa “bidhaa” zilizoporwa wakati wa ukoloni kutoka Tanzania na nchi zingine za Afrika na kwenda kuhifadhiwa kwenye majumba ya makumbusho Ujerumani.

Mbali na mafuvu, Ujerumani pia imepanga kurejesha baadhi ya mabaki ya mifupa ya wanyama na mijusi mikubwa wakubwa wanaoaminika kuwepo Tanzania miongo mingi iliyopita.

Pia nchi hiyo imeahidi kurejesha mali za asilia ambazo ziliporwa, ikiwamo vito na mapambo kutoka kwenye nyumba za machifu na watawala wa makabila ya Tanzania.

Historia inaonyesha kwamba Ujerumani ilikuwa na utaratibu wa kupora mafuvu ya baadhi ya watu “waliowasumbua” kwenye utawala wao wa kikoloni baada ya kuwaua kwenye mapigano.

Taarifa kutoka Serikali ya Ujerumani iliyopatikana chumba cha habari cha Pambazuko, zinaeleza kuwa zoezi la kurejesha mafuvu na mali zingine zilizoporwa na Ujerumani, litagarimiwa na kusimamiwa kwa uangalifu kubwa na nchi hiyo hadi kukabidhiwa kwa Serikali ya Tanzania.

Hata hivyo, taarifa haielezi lini zoezi hili litafanyika, ingawa inaaminika ni hivi karibuni.

Ujerumani inaeleza kuwa imeamua kurejesha mafuvu hayo na mali zingine za asili zilizoporwa Afrika kwa lengo la “kuendelea kuimarisha uhusiano na nchi zilizokuwa makoloni yake.”



**Chifu Mkwawa**

Miongoni mwa mafuvu maarufu yaliyoporwa na Ujerumani ni yale ya machifu wa makabila ya Tanzania (wakati huo ikiitwa Tanganyika) – likiwamo lile maarufu la kiongozi wa kabila la Wahehe, Chifu Mkwawa wa Iringa.

Chifu Mkwawa ambaye jina lake halisi ni Mtwa Mkwawa Mkwavinyika Ndevalagosi Simkali Seligamba ama wengine wakimtaja kuwa Chifu Mkwavinyika Munyigumba Mwamuyinga, alijua baada ya kuona dalili za kuzidiwa vita na Wajerumani ili kuepuka “aibu” ya kukamatwa.

Aliamua kukatiza maisha yake akiwa na miaka 43 baada ya kuongoza mapambano dhidi ya Ujerumani akikataa kutawaliwa na wageni. Alizaliwa mwaka 1855 na akajua Julai 19, 1898.

Fuvu la kichwa cha Chifu Mkwawa lilirudishwa Tanzania Juni 19, 1954 na sasa limehifadhiwa makumbusho kijiji cha Kalenga, Iringa.

Makumbusho ya Taifa la Ujerumani yaliyoko Jiji la Berlin, pia kuna mabaki ya mjusi mkubwa maarufu kwa jina la Kiingereza ‘Dinosaur’ ambaye ni kivutio kikubwa cha utalii katika jumba

## **Mafuvu 200 yaliyoporwa na Ujerumani kurejeshwa Tanzania**

hilo ambapo idadi kubwa ya watalii hutembelea kuona ukubwa wake na maelezo kumhusu. Inasadikika mabaki ya mjusi huyo yalipatikana Lindi.

Mwaka 2020, Serikali ya Tanzania kupitia ilianza mazungumzo na Serikali ya Ujerumani kuona jinsi itakavyofaidika na mapato yatokanayo na utalii kupitia mjusi huyo.

Mabaki ya mjusi huyo yanayoaminika kupatikana miaka 100 iliyoipita katika eneo la Tendaguru mkoani Lindi, yalikusanywa na kupelekwa nchini Ujerumani ambako wataalamu waliyaunganisha na kupata picha ya viungo vyake kisha kuyaweka kwenye makumbusho hiyo.

Ilielezwa kuwa lengo la mazungumzo hayo ilikuwa ni kutaka kujua kiasi gani cha mapato yanayokusanywa na namna gani wanavyoweza kugawana mapato hayo yatokanayo na watalii kupitia mjusi huyo baina ya serikali hizo mbili.

Pambazuko linazo taarifa kuwa baada ya mazungumzo hayo, Ujerumani ilipendekeza kuamua kurejeshwa mabaki ya mjusi huyo ili awepe Tanzania, ardhi yake ya asili.

Inadaiwa kuwa baada ya mwelekeo huo wa Ujerumani, baadhi ya maofisa wa wizara ya utalii, waliibuka na mapendekezo kwamba mabaki hayo yabaki hukohuko, lakini kuwepo na gawio la mapato kutokana na utalii.

Kwamba viongozi hao wa wizara walieleza kwamba sehemu kubwa ya mifupa ya mjusi huyo ni maaluma na kwamba imeungwa kwa "utaalamu wa hali ya juu" kiasi cha kuhofia sura na umbo lake kubaki kama lilivyo wakati wa "purukushani" za kusafarishwa.

Mifupa ya mjusi huyo iliyoungwa kitaalamu, imemfanya kuwa na urefu unaokadiriwa kufikia mita 13.7 kwenda



*Mifupa ya mjusi mkubwa kutoka Tanzania anayehifadhiwa Berlin, Ujerumani na kuwa kivutio cha utalii*

juu.

Hata hivyo, pamoja na jitihada za Pambazuko kutaka kujua mapato halisi ya utalii kutokana na kuwepo kwa mjusi huo, ziligonga mwamba baada ya kukosa ushirikiano kutoka Bodi ya Utalii ya Ujerumani.

Ujerumani ni miongoni mwa nchi wafadhili zinazosaidia kutunza na kuhifadhi baadhi ya malikale nchini Tanzania – ikiwamo maeneo ya asili ya Bagamoyo na Zanzibar.

Tayari Ujerumani imerejeshwa mapambo na vito vya thamani vilivyokuwa ndani ya jumba la Mfalme wa Kabila la Ogoni, nchini Nigeria. Zaidi ya Ogoni mapambo 800 yaliyoporwa yamerejeshwa Nigeria.

Mbali na Nigeria, Namibia pia ni miongoni mwa nchi za Afrika ambazo tayari zimepokea mabaki ya mafuvu na bidhaa zingine za kale kutoka Ujerumani ambazo ziliporwa na nchi hiyo wakati wa ukoloni.

Namibia ambayo ilikaliwa na Ujerumani kwa miaka mingi, inatajwa kuwa mali zake za kale nyingi ziliporwa na mkoloni wake, Ujerumani.

---

**Hakimu Handeni auawa kwa mawe****Na Scovya MANASE**

**M**APANGA, mawe na silaha zingine za jadi, juzi – Jumamosi, vilitumiwa na wananchi wanaoelezwa kuwa na hasira kali, kumuua Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Handeni, Joachim Mwakyolo kwa tuhuma za “kuvamia shamba la kijiji.”

Hakimu Mwakyolo, ambaye alikuwa likizo, alikwenda Kijiji cha Kibole, Halmashauri ya Busokelo, Rungwe, mkoani Mbeya kwa ajili ya mapumziko ambako ndiko mauti yalimkuta baada ya kushambuliwa na wanaodaiwa kuwa wanakijiji wa eneo hilo.

Mkuu wa Wilaya (DC) ya Handeni, Tanga, Siriel Mchembe alithibitisha kutokea kwa kifo hicho cha hakimu wa wilaya yake na kwamba alipokea taarifa kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dkt. Vincent Anney, ambako kumetokea tukio hilo.

“Nimepokea taarifa kutoka kwa DC Rungwe Dkt. Vincent Anney kwamba alfajiri ya leo (juzi), Hakimu Joachim Mwakyolo wa Mahakama ya wilaya hapa Handeni ameuawa na wananchi wenye hasira kali huko Busokelo,” alisema kwa sauti yenye kuashiria masikitiko.

Akielezea namna tukio hilo lilivyotokea, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dkt. Vincent Anney amesema watu watatu walienda Kijiji cha Kibole, Busokelo na kuingia kwenye shamba linaloelezwa kuwa la kijiji hicho, miongoni mwao ni hakimu wa mahakama ya wilaya ya Handeni.

Taarifa kutoka Busokelo zinaeleza kuwa hakimu huyo na wenzake, waliingia kwenye shamba hilo la kijiji ambalo lilikuwa na mgogoro ambao ulimalizwa na Mahakamani Kuu Desemba, 2022 baada ya kesi hiyo kusikilizwa mahakamani kwa miaka zaidi ya 10. Katika shauri hilo, Hakimu Mwakyolo alishindwa na kijiji baada mahakama kumuua kuwa kijiji ndiyo wamiliki halali.

Baada ya wananchi kuwaona kwenye shamba hilo, inaelezwa kuwa walikwenda kuwauliza maswali – kwanini wamo



*Mkuu wa Wilaya (DC) ya Handeni, Tanga, Siriel Mchembe*

shambani wakati kijiji hakujui ujio wa wageni wowote. Kwamba katika kujibizana, mmoja wa walioambatana na Hakimu Mwakyolo, alifyatua risasi na kujeruhi wanakijiji wawili na hapo ndipo kukatokea vurugu kubwa.

Inadaiwa kuwa wanakijiji waliona Hakimu Mwakyolo na wenzake wakichimbia ardhini kile wanachoeleza kuwa ni “vitu kadhaa” ambavyo wengi wanaamini ni ushirikina ili kushinda rufaa kuhusu umiliki wa shamba hilo. Inaelezwa kuwa hakimu huyo hakuridhika na uamuzi wa mahakama hivyo, alikuwa mbioni kukata rufaa.

Katika vurugu hizo, mmoja wa watu waliokuwa wameambatana na Hakimu Mwakyolo, alifanikiwa kukimbia, huku hakimu na mtu mwingine wakiuawa kwa mapanga, mawe na silaha zingine za jadi zilizotumiwa na wanakijiji.

Rungwe ni miongoni mwa wilaya zinazoongoza kwa migogoro ya ardhi nchini Tanzania na kuwepo kwa ripoti za matukio ya mauaji yanayotokana na “kugombea” ardhi kwa ajili ya makazi, malisho na hata shughuli za kilimo.

Tayari Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wake kuhusu tukio hilo na kwamba taarifa rasmi itatolewa na jeshi hilo kwa wananchi baada ya kazi kukamilika.

## Mwanafunzi IST aokoa wenye usonji

**Na Tryrukia MFINANGA**

**M**RADI wa kuhudumia watoto wenye usonji, umepokea msaada wa shilingi milioni 100 kutoka kwa mwanafunzi wa kidato cha nne wa Shule ya Sekondari ya Kimataifa ya Tanganyika (IST), Madeleine Kimario.

Fedha hizo zilikabidhiwa Jumatano iliyopita – Januari 18, 2023 kwa taasisi inayohusika kuhudumia watoto wenye changamoto ya usonji; Lukiza Autism Foundation kupitia kwa mkurugenzi wake, Hilda Nkabe.

Imeelezwa kuwa fedha hizo zitanufaisha baadhi ya watoto katika Kituo cha Msimbazi Mseto, Ilala, Dar es Salaam na kwamba matumizi makubwa ya fedha hizo yatakuwa ni kutekeleza mradi wa kutoa huduma za mazoezi tiba kwa wenye usonji kwa mwaka mmoja.

Taarifa zilizotolewa na taasisi hiyo zinaeleza kuwa mradi huo utashirikisha wataalamu wa mazoezi ambao watakuwa wakifanya kazi ya kuhakikisha watoto wenye changamoto ya usonji wanapata afueni kubwa.

Usonji (autism spectrum disorder -ASD) ni ugonjwa wa neva unaoathiri zaidi milango ya fahamu katika ukuaji wa mtoto. Hata hivyo, ugonjwa huo unaweza kumpata mtu yeyote bila kujali umri. Dalili kubwa za ugonjwa huu, mara nyingi haunza kubainika kwa watoto kuanzia mwaka mmoja na nusu hadi miwili.

Madeleine, mwanafunzi aliyekusanya fedha hizo, amesema kuwa aliamua kufanya hivyo ili kuhakikisha kuwa watoto wenye uhitaji maalumu, hasa wenye usonji wanapaswa kusaidiwa na jamii, na siyo familia zao pekee.

Amesema fedha zilizokusanywa zimetoka wa familia, marafiki zake, kampuni na taasisi ambazo ziliunga mkono wazo lake la kusaidia watoto wenye changamoto ya usonji. Amewashukuru wote waliosaidia kufanikisha nia yake hiyo.



*Mwanafunzi wa IST, Madeleine Kimario, katikati, akimkabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 100 Mkurugenzi Mtendaji wa Lukiza Autism Foundation, Hilda Nkabe. (Picha na millardayo.com).*

Ofisa Elimu Maalumu Mkoa wa Dar es salaam, Swalehe Msechu ambaye alipata wasaa wa kuzunguma wakati wa hafla ya kukabidhi hundi ya mfano – yenye kuonyesha kiasi cha Sh. milioni 100 zilizotolewa na Madeleine, aliuhakikishia umma kwamba serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wanafunzi wenye uhitaji maalumu, wakiwamo wale wenye usonji.

Msechu pia aimeiasa jamii kuacha imani ptofu kuhusu watoto wenye usonji na watu wote wenye mahitaji maalum kwani changamoto za afya walizonazo hazitokani na ulozii.

Ofisa huyo wa elimu maalimu amewasisitiza wazazi na walezi kuacha kuficha nyumbani watoto wenye usonji au wenye mahitaji maalum, na badala yake wapelekwe shuleni ambako wanaweza kupata usaidizi kulingana na mahitaji yao.

Akitoa shukurani kwa Madeleine na wadau wote waliofanikisha kukusanywa kwa kiasi hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa Lukiza Autism Foundation, Hilda Nkabe amesema kupatikana kwa fedha hizo kusaudua kuimarisha afya za watoto wenye usonji kwa kiasi kikubwa kwani zitasaidia katika mawasiliano na mazoezi tiba na kutosa mwito kwa Watanzania wengine kuendelea kuchangia watu wenye mahitaji maalum.



---

## **Kutendea haki sawa kwa walio sawa**

**Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA**

**K**ATIKA makala zilizopita niliwahi kutaja kanuni hii; kuwatendea haki sawa walio sawa, ambayo inabeba ujumbe mzito.

Sasa ni vyema vyema kuipa nafasi zaidi kuijadili na ikiwezekana kutoa na mifano ili kujenga uelewa zaidi. Kwa wale ambao wamebobeza katika masuala ya haki jamii wavumilie na kukubali kutembea nasi kwa mwendo huu.

Kanuni hii ni tofauti na ile ya kutenda haki sawa kwa watu wote. Haki sawa ni nadharia pana ambayo naweza kusema ni kama inabeba hizi zingine zote.

Haki sawa hapa maana ni usawa katika haki za msingi kama vile kuwa na haki sawa mbele ya sheria, kuishi, heshima ya utu, na maeneo mengine. Kwa lugha nyingine niseme kwamba hizi kanuni zingine, pamoja na hii tunayojadli leo, zinafanua kanuni pana ya haki sawa kwa watu wote yaani usawa wa haki za msingi.

Kanuni ya kutenda haki sawa kwa walio sawa inalenga kusawazisha usawa katika makundi yaliyo sawa. Kanuni hii hulinda upendeleo wa namna mbalimbali kwa mfano ukabila, udini, kiitikadi, kitaaluma, rangi, na sehemu zingine.

Huduma za kijamii na fursa zilizopo zitolewe na kugawanywa sawa. Kanuni hii huwa ngumu kutekelezwa katika jamii zile ambazo rushwa na upendeleo vimekuwa ndio kanuni ya maisha ya kila siku.

Zipo jamii ambazo mambo hawaendi na milango ya fursa hufungwa kwa watu ambao hawana watu ama “wanaowapigia vifua” au “wanaowakingia vifua”. Ili kufafanua kauli hii nitoe mifano miwili.

Tunasikia manung’uniko mara kwa mara pale ambapo vijana wawili wamemaliza masomo yao na kujipatia shahada. Mmoja ametoka katika familia



### **Haki**

ambayo huko juu katika serikali, mashirika na kampuni ana kundi la watu wakubwa ambao ni ndugu zake anaofahamiana nao.

Ambapo kijana wa pili katoka katika familia ya kawaida isiyo na vigogo, ambaye hata kusoma kwake kumegharimu sana jasho la wazazi wake hata familia nzima kufunga mikanda.

Kati ya vijana hao wawili zinapotangazwa nafasi za kazi na wote wakaomba katika jamii yetu hutokea mara nyingi kwamba yule mwenye vigogo huko juu hupata ajira kirahisi.

Tena yawezekana kwamba yule aliyetoka katika familia ya kawaida amefanya vizuri sana chuoni na anao uwezo na sifa za kupata ajira na kufanya vizuri, lakini kwa kuwa mfumo wa haki katika jamii una matobo, basi milango ya fursa imefungwa kwake. Kwa yule kijana mwingine milango yote ya fursa iko wazi.

Haijalishi hata kama uwezo wake ni mdogo bali maadam ana watu huko juu, basi mambo ya ajira humnyookea kirahisi. Huu ni mfano mmojawapo ambao tunaona kuwa kanuni ya kutenda haki sawa kwa walio sawa imevunjwa.

---



## **Chadema waja na mpango mkakati ‘kupindua meza’**

**Na Mwandishi WETU**

**B**AADA ya zuiu lisilokuwa la kikatiba wala kisheria, la mikutano ya hadhara kwa muda mrefu, sasa ni wazi kwamba, Chadema wamezindua mikutano yao ya hadhara wakiwa na lengo kubwa la kueleza wapi serikali “imekwama” kukomboa wananchi na janga la ufukara.

Mtangulizi wa Rais Samia Suluhu Hassan, John Pombe Magufuli, miaka saba iliyopita, alitoa kauli kuzuia mikutano ya hadhara, ambayo ni injini ya kuendesha na kukuza vyama vya siasa.

Rais Magufuli, bila kupima umuhimu wa kidemokrasia kuendesha nchi, alitumia ubabe wa kiutawala kueleza tu; “sasa hakuna mikutano ya hadhara ya vyama,” na ikawa sheria.

Hatua hiyo ilifuatiwa na madhila mengi kwa wanasiasa, waandishi wa habari, wafanyabiashara na watu wa kada nyingine, ikiwamo kuumizwa, kutekwa, kuteswa, kupotezwa na wengine kuminywa uhai wao.

Rais Samia kwa mabadiliko ya sasa ya kuruhusu kuwepo kwa mikutano ya hadhara na kuacha demokrasia ipumue na kuendelea kukua, unatoa mwanya wa serikali kusemwa na kukosolewa ili ijirekebisha mahali itakapokuwa imekosea.

Tayari, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kupitia kwa mwenyekiti wake, Freeman Mbowe, kimepongeza hatua ya Rais Samia kuvunja zuiu hilo linaloelezwa na wengi kuwa “haramu.”

Ni kwa msingi huo, Chadema wanakuja na nadharia zenye kubeba hatua kadhaa za kuinyoshea serikali kidole kwa utendaji wake.

Nadharia hizo zinaweza kuwekwa katika hatua tatu za mabadiliko ya kifikra,



*Freema Mbowe, kiongozi wa upinzani*

kisera, kisheria, na kitaasisi.

Mosi, ni kutengeneza “tasnifu asilia -” (thesis) kwa kuhakikisha kwamba, hali ya mfumo uliopo kwa sasa, yaani mtazamo rasmi unaokubalika kwa sasa, unachambuliwa vizuri.

Pili, ni kutengeneza “tasnifu kinzani -” (antithesis) kwa kuhakikisha kwamba, matatizo yaliyomo katika mfumo wa sasa yanabainishwa sawasawa, ili tasnifu asilia iweze kukosolewa kwa usahihi na kwa uhakika, kwa kutumia ushahidi.

Na tatu, ni kutengeneza “tasnifu hitimisho -” (synthesis) kwa kuhakikisha kwamba, kambi zinazopingana zinafikia mwafaka, kwa kuzalisha fikra, sera au sheria inayokubalika kwa kambi zote, kwa sababu ya ushahidi uliowekwa mezani na kushuhudiwa na kambi zote, wakati wa mchakati wa majadiliano.

Katika hatua ya tatu, mrejesho kutokana na tasnifu kinzani hufanywa sehemu ya tasnifu asilia ili kuzalisha tasnifu hitimisho, inayokubalika kwa kambi zote.

Kisha, mduara wa tasnifu asilia, tasnifu kinzani na tasnifu hitimisho hujirudirudia hadi kuunda mchakato wenye

## **Chadema na mpango mkakati**

**Inatoka Uk. 9**

muundo wa “spairo” (spiral), kila duara la spairo likiwapeleka wahusika karibu zaidi na ukweli.

Hotuba zilizotolewa na viongozi wa Chadema, Januari 21, 2023, katika uwanja wa Furahisha, Jiji Mwanza, zinathibitisha kwamba, nadharia ya udayalektika kuhusu mabadiliko ya kijamii imeanza kutekelezwa na Chadema.

Katika kuweka uzito kwenye nadharia hizo tatu, Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, alilikutubia taifa jioni ya siku hiyo alisema yafuatayo;

“Serikali ya awamu ya tano ililigeuza taifa hili kuwa taifa la maumivu, mateso na misiba...

...Nikiri kwamba sisi sote tulioumizwa na mateso ya viongozi wetu, wana Chadema wameumizwa, wana CCM wameumizwa na wapo wana CCM walionufaika na mateso hayo...

... Taifa letu halipaswi kuwa taifa la kuumuza kiongozi yoyote, mwanachama yoyote, mfuasi yeyote wa chama chochote. Taifa letu linapaswa kuwa taifa la watu walioungana, wanaoshikamana, wanaosimama katika misingi ya demokrasia...

... Taifa hili limepitia mengi, taifa hili linapaswa kuwa na watu ambao wameungana, wameshikamana na kusimama katika misingi ya demokrasia, utawala wa sheria na haki kwa wote...

... Ninaposimama nikiwa mwenyekiti na kiongozi wa Chadema kudai haki, sisimami kwa ajili wa wana Chadema, bali nasimama kama kiongozi wa kudai haki za watu wote...

... Naomba nilisitizite sana, tusijenge tabia ya kuwachukua wanachama wa CCM kwa sababu ya madhila tuliyopitia. Wajibu wetu ni kuwashurutisha kwa hoja ili watambue, ndani ya Chadema kuna haki, ustawi na fursa ya kumsaidia kila mmoja na akawa raia mwema kwa nchi



**Rais Samia Suluhu Hassan**

yetu...

... Tunahitaji kukaa kama nchi kutambua kwamba nchi hii haiwezi kuendelea kwa kuigawanya vipande vipande. Eti kuna na kipande cha Chadema, kuna kipande cha CCM, kuna kipande cha UDP...

... Chadema tuna kauli kuu inayosema ‘no hate, no fear’ (hakuna chuki, hakuna woga). Natangaza wazi kuwa chama hiki siyo chama cha chuki. Hatuwezi kujenga utaiwa wa nchi hii kwa kujenga chuki...

... Dhana ya ‘no hate’ (hakuna chuki), iambatane na dhana kwamba hatumuogopi mtu...

... Nampongeza Rais Samia Suluhu kwa kukubali maridhiano. Wapo watu wanatamani maridhiano yasanikiwiwe. Wao wanafaidi maisha nje ya maridhiano. Samia alikubali nia ya maridhiano kinyume na matakwa ya chama chake...

... Kwa pamoja tuna wajibu wa kujadiliana yapi ni mambo ya misingi ya kuyafanya ili kulipeleka taifa letu katika furaha, ustawi na haki kwa kila mtu...

... Katika miaka yangu 30 ya kupigania taifa hili, natamani nitakapoacha uongozi, niache taifa langu, nchi yangu, watoto wangu, wajukuu wangu wakiwa wanapendana, wanaoshikamana na kuitafuta kesho yetu pamoja.”

Ni kwa maneno ya Mbowe, kuna kila

**Inaendelea Uk. 11**

## **Chadema na mpango mkakati**

*Inatoka Uk. 10*

dalili kwamba siasa za “kunyukana na kuingiana vifua” huenda zinaondoka Chadema na kuja na staili nyingine ya mapambano ya siasa kwa lengo la kuongoza Tanzania.

Hata hivyo, wapo baadhi ya wahafisdhina ndani ya Chadema kwa hatua hii wanaona kama mwenyekirti wao, Mbowe amewasaliti na kutaja kwamba “huenda amelamba asali.” Hatua ambayo Mbowe amekimea na kulaani wanaosambaza uongo kwamba amepokea rushwa kutoka kwa wapinzani wao ili “kumlainisha.”

Katika hotuba hii, Mbowe ameongelea mambo matatu.

Mosi, Mbowe anaongelea tasnifu asilia, isemayo kwamba, kuna wafuasi wa chama tawala ambao, tangu serikali ya awamu ya tano, wamekuwa wafuasi na watetezi wa mfumo wa kisiasa unaokuza na kuhami maslahi ya wachache na kutelekeza maslahi ya wengi.

Huu ni mfumo uliokweza dhuluma na kutweza haki, mfumo wenye kutukuza chuki dhidi ya wapinzani badala ya kufanya urafiki nao.

Ni mfumo ulioongozwa na imani hasi kwamba, ukosoaji wa mifumo iliyopo kwa lengo la kuibua ukweli mpya, na hivyo kujenga mifumo bora zaidi, siyo njia halali ya kusukuma gurudumu la maendeleo.

Ni mfumo uliotukuza ubaguzi wa kikanda na kiitikadi na kusahau kuimarisha umoja wa kitaifa bila kujali itikadi, ukabila na ukanda.

Pili, Mbowe anaongelea tasnifu kinzani, isemayo yafuatayo; kwamba, kwa mujibu wa ndoto ya waasisi wa nchi yetu, Tanzania ni taifa linapaswa kuongozwa na serikali inayopigania maslahi ya watu wote, badala ya kuhangaikia maslahi ya watu wachache.

Kwamba, Tanzania ni taifa linapaswa kukumbatia mifumo inayokweza haki na

kutweza dhuluma, inayotukuza urafiki badala ya kujenga uadui.

Kwamba, Tanzania ni taifa linapaswa kukumbatia mifumo kuongozwa na kanuni kwamba, ukosoaji wa mifumo iliyopo kwa lengo la kuibua ukweli mpya, na hivyo kujenga mifumo bora zaidi, ndiyo njia pekee ya kusukuma gurudumu la maendeleo.

Kwamba, Tanzania ni taifa linapaswa kupinga ubaguzi wa kikanda na kiitikadi na kuimarisha umoja wa kitaifa bila kujali itikadi, ukabila wala ukanda.

Na tatu, Mbowe anaongelea tasnifu hitimisho, isemayo yafuatayo; kwamba, kazi ya kujenga nchi, katika mazingira ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi, inapaswa kufanyika kwa mujibu wa kanuni kwamba, ukosoaji wa mifumo iliyopo kwa lengo la kuibua ukweli mpya, na hivyo kujenga mifumo bora zaidi, ndio njia pekee ya kuleta haki ya kweli, amani ya kweli, uhuru wa kweli na maendeleo ya kweli nchini Tanzania.

Tasnifu hitimisha inayoongelelwa na Mbowe, inaakisi hoja ya Profesa Euphrase Kezilahabi, kama ilivyotolewa mwaka 1978, kupitia tamthiliya yake iitwayo “Kaptura la Marx.”

Tamthiliya ilishutumumu ukiritimba na matumizi mabaya ya madaraka katika mfumo wa Ujamaa uliouanzishwa enzi za Mwalimu Julius Nyerere, aliyekuwa Rais wa Tanzania.

Kwa mfano, ndani ya kitabu “Kaptura la Marx (1999),” kwenye ukurasa wa 20, maelezo ya mhusika Korchnoi Brown kwa Raisi Kapera na mawaziri wake kuhusu njia ya kufikia nchi ya usawa yanasomeka hivi;

“Mtakwenda. Halafu mtapinda, mtapinda tena, halafu tena mtapinda, mwishowe mtapindapinda hadi mtakapofika mabonde yenye matope. Mtapita katikati ya matope.

“Halafu milima, halafu misitu yenye

*Inaendelea Uk. 12*

---

## Chadema na mpango mkakati

*Inatoka Uk. 11*

miiba hadi mtakapofika jangwani. Kutoka jangwani mtaingia tena bondeni chini kwa chini hadi baharini. Hakuna mitumbwi wala ngalawa.

“Mtaogelea, ingawa kuna papa wengi. Mkishavuka mtafika nchi iitwayo Svoboda. Kabla ya kuondoka katika nchi hii itawabidi kupambana na majitu yanayofanana na mimi. Mkitoka hapo mtafika kwenye njia nyembamba.

“Hawa (mawaziri) hawatapita hawa. Njia hiyo itawafikisha katika nchi iitwayo Fraternite. Kutoka Fraternite mtafika Usawa. Ulizeni tu watu watawaonyesha.

“Mkifika Usawa mtawakuta Waswahili wenzenu wameketi nje ya Ikulu ndogo ya Ravensto.”

Neno “Korchnoi” ni jina la Kirusi, “Brown” jina la Kiingereza. Majina haya yanarejea njia ya Tanzania ya Nyerere kati ya “mashariki” ya kikomunisti na “magharibi” ya kibeberu.

Neno “Fraternite” ni msamiati wa Kifaransa wenye kumaanisha “undugu.” Ni moja ya tunu tatu zinazoyatambulisha mapinduzi ya Kifaransa, yaani “uhuru, usawa na undugu.”

Jina la nchi ya “Svoboda” linatokana na msamiati wa Kirusi wenye kumaanisha “uhuru.” Ni jina la nchi linalorejea wito wa mapinduzi kama yaliyofanyika Ufaransa.

Hii ni sehemu ya ushahidi kwamba, tamthiliya ya “Kaptula la Marx” ilihimiza matumizi ya mbinu za kidayalektika kuhusu mabadiliko ya kijamii, kama zilivyoasisiwa na Mjerumani Georg Hegel (1770-1831), na kisha kunadiwa na Mjerumani mwenzake Karl Marx (1818-1883).

Chadema wamechagua mbinu mwafaka, ambayo kwa sasa hutumika hata mahakamani, kulingana na mwongozo wa Profesa Stephen Toulmin (1922-2009), wa Uingereza.



Tundu Lissu

Katika kitabu chake, “The Uses of Argument (1958),” Profesa Toulmin anasema kuwa hoja kamilifu, haipaswi kuwa na sehemu tatu kama alivyofundisha Aristotle, yaani hoja yenye “dokezo kuu, dokezo dogo na hitimisho.”

Bali, hoja iliyokamilika inapaswa kuwa na sehemu angalau sita, yaani, “tasnifu, ushahidi, waranti ya ushahidi, msingi wa waranti, tasnifu kinzani, majibu ya tasnifu kinzani, na majumuisho -” Yaani, “thesis, ground, warrant, backing, objection, rebuttal, and synthesis.” Hivyo, Chadema wamechagua barabara iliyo mwafaka.

Walizindua tena rasmi mikutano ya kisiasa baada ya kuzuiwa miaka saba iliyopita kwa njia ya tamko la aliyekuwa Rais wa Tanzania John Magufuli.

Lakini, mnamo Januari 3, 2023, Rais Samia Suluhu Hassan, aliamua kuondoa zuio hilo kutokana na maridhiano ya kitaifa yaliyoasisiwa na yeye pamoja na Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe.

## Harufu ya rushwa Mv Mapinduzi

Na Jabir Idrissa, Zanzibar

**K**UNA kitendawili hakijateguliwa na Kutawala au uongozi wa Zanzibar na kwa vile wenye mamlaka wanavyopiga danadana kila swali linapoulizwa kuhusu hatima ya “ufisadi mkubwa” uliofanywa miaka kadhaa iliyopita.

Ni kutokana na kukwepa huko kujibu ama kutegua kitendawili, mtu anapata shaka kama kweli pana utashi wa uongozi kukomesha ufisadi serikalini.

Hiyo ndio hali halisi ya mambo na mwenendo mzima katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa kwa mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), chini ya Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi, ambaye kwa matamshi amejipambanua na kujenga imani kwa wananchi kuwa “nachukia sana rushwa.”

Shaka ya wananchi na hususan wapambanuzi na wachambuzi wa masuala ya kiutawala, inatokana na kasi isiyotosha ya kupambana na ufisadi ambao unajulikana ulivyo tatizo kubwa kwa mataifa ya Afrika.

Ni kweli isiyoshaka kwamba Rais Dkt. Mwinyi alichukua mapema agenda ya kukomesha ufisadi baada ya kuibuka na kutangaza “sitakuwa na muhali hata chembe na walarushwa kwa kuamini rushwa ni ‘adui wa haki’ na inaumiza uchumi wa nchi, hivyo kuikwamisha serikali kwenye tope zito katika azma ya kumaliza tatizo hilo la ufisadi.

Suala lenyewe lipo hivi; mwandishi anamuuliza Rais Dkt. Mwinyi anaonaje mkazo mkubwa katika kupambana na ufisadi ukawekwa kwenye kushughulikia “rushwa kubwa” kwa kuwa inaaminika ndiyo inayoumiza zaidi uchumi wa taifa na kuvuruga msingi wa kuinua ustawi wa jamii?

Anaulizwa kiongozi haoni kuwa kuweka nguvu kubwa kwa wale wanaochukua rushwa ndogo serikali inachelewesha azma ya kukomesha ufisadi mkubwa kwa vile hata wananchi wataona hakuna umakini katika



*MV Mapinduzi II*

kutekeleza dhamira ya serikali.

Swali la kuhimiza kudhibiti rushwa kubwa linaletwa kwa kuzingatia kuwa mpaka leo ikiwa ni miaka miwili ya uongozi wa awamu ya nane, hajapelekwa mahakamani mtuhumiwa wa rushwa kubwa badala yake wanapelekwa “vidagaa” huku walarushwa kubwa wakiendelea kutanua mitaani.

Kwamba serikali hajaona haja ya kubana wale “wakubwa” waliohusika na ununuzi wa meli ya Mv. Mapinduzi II iliyotamkwa hivi karibuni kuwa “haiuziki?”

Hii meli ambayo Rais Dkt. Mwinyi ametamka kuwa haiuziki, baada ya hapo nyuma kidogo kusema “Serikali sasa tumeamua meli zote ziuzwe ili tuanze upya kwa kununua mpya zinazotufaa kwa mazingira ya kwetu” ilinunuliwa mwaka 2016 kwa Sh. bilioni 40 na kabla ya kuanza safari ya kutoa huduma ikapelekwa chelezoni Mombasa, Kenya ambako zilitumika Pauni za Uingereza 90,000, na hapa bado gharama za kuhudumia wafanyakazi waliokwenda nayo huko.

Ilitumika kwa miaka miwili na ikaonekana haiwezi tena kutoa huduma. Lakini wakati inatengenezwa nchini Korea Kusini, kamati iliyosimamia ununuzi ikiongozwa na aliyekuwa Waziri wa Fedha, Omar Yussuf Mzee, ilipiga picha na kuzirusha mitandaoni kuonesha kuwa meli mpya ndiyo inatengenezwa.

Isitoshe, ilipoletwa nchini na kuandaliwa sherehe kubwa, rais wakati

---

## Harufu ya rushwa Mv Mapinduzi

*Inatoka Uk. 13*

ule, Dk. Ali Mohamed Shein baada ya kuelezwa na hao wasaidizi wake walionunua meli, alitangaza kuwa “haiwezekani watupe meli kongwe maana (watengenezaji) hawawezi kutudanganya serikali wala shirika la kimataifa la usimamizi wa usafiri wa baharini (IMO).” Anakazia kuwa meli iliyonunuliwa na wasaidizi wake ni mpya wala siyo mbovu.

Wakati watengenezaji wakiendelea kufanyia kazi “meli mpya” na hasa pale meli ilipokuwa njiani kuletwa nchini, zilivuja taarifa na zikaenea kwingi kuwa meli inayoletwa siyo mpya na kwamba “serikali imeuziwa mtumba” ila wasimamizi walishikilia kumdanganya rais wakati ule wakisema; “mheshimiwa usikilize wapinzani hawana sera. Tumenunua meli mpya na siyo muda mrefu uongo wa wapinzani utathibitika.”

Mv Mapinduzi II ilipowasili bandarini Malindi, mjini Zanzibar watu wakaamini labda ni mpya kweli. Kilichotokea na sasa kuwa meli hii “haiuziki” ndio mtihani kwa walionunua na wale wanaopata uzito leo kuwabana hao inaodhihirika kuwa walimdanganya rais wakati ule na wakadanganya umma wa Wazanzibari ambao wameuziwa ‘mbuzi kwenye gunia.’

Hoja anayojenga mwandishi muliza swali kwa Rais Dkt. Mwinyi ni kwamba yumkini waliosimamia ununuzi wamelipwa malipo haramu ya rushwa kuchukua meli kongwe kwa pesa nyingi zilizofaa kununua meli mpya.

Na sasa meli haiuziki kwa sababu hakuna aliyeshawishika kuinunua hata kuifanya chuma chakavu. Kiko wapi kitendawili?

Kitendawili ni kwamba wananchi walidanganywa wakati viongozi wao waliponunua meli mbovu kwa pesa nyingi na inathibitika miaka mitano tangu inunuliwe, huku ikiwa imefanyakazi kwa miaka miwili tu. Leo hakuna anayeitaka.

Viongozi wa leo wanajitahidi kukwepa kuwabana wale waliodanganya juzi. Hili swali la kwamba “kuna uchunguzi

unaofanywa” halijibiwi. Hakuna aliye tayari kulijibu - siyo waziri anayehusika na sekta ya mawasiliano na usafirishaji wala Mamlaka ya Kuzulia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu.

Kutokana na ukimya huo, idadi kubwa ya wananchi wanaamini kuna dalili za kulindana kwa wakubwa kwa kuwa wanatambuana juu ya ‘dhambi’ zao – na hasa kuhusu swala la rushwa na kuminya haki za binadamu.

Hivi ni kitu gani kinashindikana kutaja kwamba huyu na yule ndiyo wahusika wakuu wa kununua meli ile na kwamba uchunguzi dhidi yao unaendelea na utakamilishwa kwa muda fulani.

Uhakika ni kwamba ununuzi wa meli ya Mv Mapinduzi II haukuzingatia kile kinachoitwa – ulinganifu wa fedha na thamani ya kitu kinachonunuliwa (Value for Money) – hivyo, huenda kuna rushwa ilitembea.

Alipoulizwa swali Rais Dkt. Mwinyi mwezi uliopita, pakikaziwa hoja kuwa meli ya 2016 haiuziki leo 2023, lakini nyuma kidogo serikali ilitangaza kufanikiwa kuuza Mv. Maendeleo kwa dola za Marekani 230,000 (thamani yake halisi ni Dola 370,000 kwa mujibu wa wathamini wa serikali) wakati hii ilinunuliwa miaka ya 1970. Rais Dkt Mwinyi alisema mwandishi hajafanya utafiti.

Nilidhani hakuna rushwa kwenye uuzaji wa Mv Maendeleo iliyochakaa na ambayo imewekwa sokoni baada ya kulipwa Sh bilioni 1.5 za gharama za maegesho chelezoni Mombasa. Kwa kuwa hakuna anayetoa maelezo yaliyonyooka, naambiwa nikubali maelezo ya Rais ambaye akishasema hakuna wa chini yake awezaye kubadili maneno.

Je, unapoufuata mtiririko huu wa maelezo, utaamini wananchi “hawakupigwa” na hivyo waendelea na maisha yao na kuamini “serikali yao, kiongozi wao?”

*Mie nasubiri uchunguzi.*

---

# **Pambazuko**

**Gazeti la Pambazuko sasa  
kupokea matangazo**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi kwa

kuwasiliana kupitia namba hii:  
**0744 768 263** au Barua- Pepe;  
[info@pambazuko.tz](mailto:info@pambazuko.tz)

*Karibu sana Pambazuko isaidie  
kupaisha na kupambazua  
huduma na biashara yako.*



---

## Rais Biden aingia matatani

**R**AIS wa taifa lenye nguvu kubwa za kijeshi na kiuchumi duniani, Marekani, Joe Biden sita aingia matatani baada ya kupatikana kwa nyaraka za siri kwenye makazi yake binafsi, Mji wa Wilmington, Delaware.

Taarifa ambazo zimepatikana jana kutoka Marekani na kuthibitishwa na shirika la upelelezi la nchi hiyo, FBI, zinaeleza kuwa nyumba ya Rais Biden ilikutwa na nyaraka sita zaidi juzi, baada ya kupatikana zingine wiki iliyopita katika makazi hayohayo. Idadi hiyo inafanya nyaraka zilizochukuliwa kutoka kwa Biden kufikia 10.

Inaeleza kuwa nyaraka hizo zilipatikana baada ya kufanyika kwa upekuzi wa kawaida katika nyumba za marais wanapokuwa madarakani au wanapokuwa ameondoka Ikulu ya Marekani, almaarufu White House.

Maofisa wa FBI wakishirikiana na wanasheria wa Biden kutoka ofisini kwake – Ikulu, wanaendelea na uchunguzi wao kutambua endapo Rais Biden amevunja sheria kwa kukutwa na nyaraka hizo zinazotajwa kuwa “muhimu.”

Imebainika kuwa nyaraka hizo zote zilikuwa zikitumika kufanya mawasiliano muhimu kati ya Rais Barack Obama na makamu wake wakati huo, Joe Biden.

Inadaiwa kuwa nyaraka hizo zimepatikana kwenye gereji ya nyumbani kwa Biden mjini Wilmington, ambako mara nyingi amekuwa akienda kwa ajili ya kupumzika mwishoni mwa wiki na nyakati za sikukuu za kitaifa.

Hatua hii ya kuchunguzwa kwa nyaraka hizo kutoka nyumbani kwa Rais Biden imekuja miezi mitatu baada ya FBI ‘kuvamia’ makazi binafsi ya Rais (mstaafu) Donald Trump, huko Mar-a-Lago, Florida na kuondoka na nyaraka zaidi ya 100 ambazo uchunguzi wake unaelekea kukamilika. Nyaraka hizo zilielezwa kuwa “za siri kubwa.”



**Joe Biden**

Tayari mwanasheria mkuu wa serikali ya Marekani, Merrick Garland amemteua mtaalamu wa kuchunguza nyaraka, Robert Hur kuchunguza nyaraka za siri katika makazi binafsi ya Rais Biden.

Aidha, Hur atachunguza pia tukio la awali la kukutwa kwa nyaraka kama hizo za siri katika Ofisi ya Rais Biden iliyoko Washington. Nyaraka hizo zinasadikika zilikuwepo kwenye ofisi hiyo tangu Biden alipokuwa makamu wa rais.

Chama cha upinzani cha Republican kimelaani kitendo cha Rais Biden kukutwa na nyaraka hizo za siri na kueleza kwamba “amekiuka kiapo chake” wakati akiingia Ikulu kuongoza Marekani na watu wake.

Chama hicho kinahoji izeje Rais Biden atunze nyaraka za siri za serikali nyumbani kwake kinyume cha sheria? Kwamba nyaraka zote za siri za taifa zinapaswa kutunzwa kwa uangalifu mkubwa ndani ya ikulu ya nchi hiyo.

Serikali ya Marekani imeeleza kuwa mchakato wa uchunguzi huo na matokeo yake utafanywa kwa uadilifu na uangalifu mkubwa kabla ya kutoa matokeo yake kwa umma wa Marekani na dunia nzima.

Habari hii imepatikana kutoka vyanzo mbalimbali vya intaneti, hasa magazeti ya Marekani.

---

## **Kada CCM ‘aliyeondoka’ na ndoto**

**Na Deusdedith KAHANGWA**

**M**ILAKA 64 iliyopita, yaani Februari 12, 1959, Revelian Rwazo na mkewe Clementina Kabeiyamu, wa Wilaya ya Karagwe, mkoani Kagera, walipata mtoto wa kiume waliyempa jina la Sabinian, baadaye akawa maarufu mitaani akiitwa Sabby, jina ambalo ameendelea nalo hadi anaaga dunia.

Sabby hadi anakutwa na mauti, amekuwa akishiriki mchezo wa kuigiza uitwao “maisha” unaofanyika katika jukwaa la ulimwengu. Ameigiza kama mzazi, mwanasiasa, mwanajamii, mwanamazingira, na mjasiriamali.

Ushiriki wake katika “igizo la maisha” ulikoma Januari 13, 2023, akiwa Hospitali ya Taifa Muhimbili, alipofariki dunia kwa sababu ya ugonjwa.

Wakazi wa Dar es Salaam wanaotoka “Karagwe Kaskazini,” yaani “Barabara ya Kayanga-Kituntu-Mabira”; “Karagwe Kusini,” yaani “Barabara ya Omurushaka-Nyaishozi-Bushangaro”; na maeneo baki ya Kagera walifika msibani Kimara, kwa ajili ya kutoa pole na kupanga mipango ya mazishi ya Sabby.

Baadaye, mwili wa Sabby ulifanyiwa ibada na kisha kupelekwa Karagwe kwa ajili ya mazishi. Mhashamu Askofu Almachius Rweyongeza, wa Jimbo Katoliki la Kayanga, iliongoza ibada ya mazishi, kijijini Rwambaizi.

Sabby atakumbukwa. Alikuwa mwanachama na mkereketwa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM); Katibu mwenezi wa CCM Wilayani Karagwe; na Katibu mwenezi wa CCM Mkoani Kagera.

Pia, alikuwa Mjumbe wa Mkutano Mkuu, CCM Taifa; Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi, CCM Taifa; Mjumbe wa Mkutano Mkuu, CCM mkoani Kagera; Diwani kwa miaka 15,



tangu mwaka 2005 hadi 2020, kwanza katani Igurwa, na baadaye katika Kata ya Kanoni.

Sabby alitumia muda wake mwingi kuhudumia jamii ya Karagwe. Alikuwa mfanyabiashara ambaye aliamini katika kutoa huduma zaidi; rafiki wa mazingira kupitia taasisi yake ya Himaya; rafiki wa mawasiliano ya redio kupitia ujumbe wa Bodi ya Radio Karagwe; na rafiki wa elimu kupitia ujumbe wa bodi katika sekondari kadhaa.

Sabby alihitimu darasa la saba mwaka 1972 katika Shule ya Msingi Rwambaizi, huko Karagwe, mkoani Kagera. Alimaliza kidato cha nne katika Sekondari ya Tarime, mkoani Mara, mwaka 1976. Sabby alioa mwaka 1983 na kupata watoto saba.

Baadaye, alipata astashahada ya kilimo nchini Uganda; na astashahada ya maendeleo ya jamii nchini Norway.

Sabby alikuwa na ndoto ya kuona majimbo mawili ya uchaguzi yakizaliwa ndani ya Karagwe. Yaani Karagwe Kaskazini na Karagwe Kusini.

Pia alitamani kuona halmashauri ya wilaya mpya inakuwepo, lakini umauti umemkuta akiwa bado na ndoto hizo.

**Buriani Sabby.**

## **Fuvu la Mangi Meli lirudishwe**

**Mhariri,**

**N**AOMBA kutoa maoni yangu kuhusu kitabu kinachoitwa “Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko Misingi na Maendeleo.”

Kitabu hiki kimeandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, mwaka huu wa 2022, na kuchapishwa na kampuni ya Mkuki na Nyota Publishers ya Dar es Salaam.

Kwenye ukurasa wa 17, kitabu hiki kinasema kwamba, wakoloni wa Kijerumani walikata vichwa vya machifu wetu wapatao 200 na kupeleka mafuvu huko Ujerumani.

Fuvu la Chifu Mkwawa lilirejeshwa Tanganyika tarehe 9 Julai, 1954, lakini, vichwa vya mashujaa wetu wengine bado havijarudishwa kutoka Ujerumani mpaka sasa.

Ni kutokana na msingi huo, inawezekana wapo machifu wengi tu ambao vichwa vyao havijarudishwa na historia yetu haionyeshi wapi walizikwa.

Ni muhimu sana kwa historia ya Tanzania kuonyesha walipozikwa machifu hawa na ama kuelezwa mabaki ya mifupa yao itarejeshwa lini kama bado iko Ujerumani.

Naomba mafuvu haya yarejeshwe.  
*Lyamuya Uronu, Moshi.*

## **Barabara Masaki zimesahaulika**

**Mhariri,**

**P**AMOJA na kwamba eneo la Masaki linatambulika kuwa sehemu wanayoishi viongozi wengi wa Tanzania, lakini bado kuna ubovu mkubwa wa barabara.

Hivi sasa barabara za maeneo mengi ya Dar es Salaam yanafanyiwa ukarabati na kujengwa kwa kiwango cha lami, lakini sioni dalili za barabara za maeneo yetu, Masaki kuanza kutengenezwa.

Naamini ubovu wa barabara za maeneo hayo zinajulikana, kwa kuwa viongozi wengi hutumia barabara hizo kwenda nyumbani ama kwenye shughuli zao, ingawa kwamba hakuna ukarabati unaofanyika, licha ya maeneo mengi kuwa na barabara nzuri kwa sasa.

Huenda hawa wakubwa hawaoni kama kuna barabara mbovu kwa kuwa wao wanatumia magari makubwa ambayo hayahisi ubovu huo.

Naomba mamlaka inayohusika kuangalia namna ya kuanza ukarabati wa barabara za Masaki, kwani sisi wenye usafiri wa umma ama wale wenye magari madogo wanateseka zaidi.

*Alfred Kaluse,  
Simu: 0767 324367*

## **Matokeo yameshtua wengi**

**Mhariri,**

**M**ATOKEO ya mitihani ya Kidato cha Pili iliyofanyika mwaka jana, hakika yamenistua.

Naamini na wengine wengi wamekumbwa na wasiwasi kwamba huenda vijana wetu hawapewi elimu inayofaa au labda mitihani inatungwa bila kufuata yale waliyofundishwa darasani.

Inasikitisha zaidi kwamba masomo wanayopaswa kuyafanyia kazi zaidi, hasa ya sayansi na hisabati ndiyo wamepata alama chache sana.

Ni wakati muafaka sasa wakuu wa serikali, na hasa wizara ya elimu kujipanga upya kuona ni namna gani wanakwamua elimu yetu.

*Masolwa Kijah, Kawe, Dar es Salaam.*

### **Tunapokea Barua**

*Mhariri anapokea barua kutoka wasomaji wake kwa ajili ya kuzichapisha ama kusitafutia majibu kutoka ofisi za serikali na binafsi. Tuma barua yako kwa njia ya barua-pepe: info@pambazuko.tz au kupitia namba ya simu: 0744 768 263*

## Neno 'ni' na maana zake kumi

Na Dionizi KAMELE

**K**ATIKA sarufi ya Kiswahili, maneno hugawanyika kwenye makundi saba. Kuna nomino, viwakilishi, vivumishi, vitenzi, vielezi, viunganishi, na vihisishi.

Neno 'ni' na kinyume chake 'siyo,' hufanya kazi kama 'kitenzi' kinachounganisha jina la kitu kinachotajwa na sifa zinazohusiana na kuwepo au kutokuwepo kwa kitu hicho.

Mfano, 'jua 'ni' kitu chenye nishati ya mwanga mkali kinacholimulika dunia kutokea angani wakati wa mchana.'

Hali ya kuwepo kwa kitu mahali fulani huitwa 'udhati wa kitu' au 'uhalisia wa kitu,' yaani 'the being of a thing.'

Na hali ya kutokuwepo kwa kitu mahali fulani huitwa 'ubatali wa kitu' au 'ombwe,' yaani 'the nonbeing of a thing.'

Kwa ujumla, neno 'ni' linaweza kubeba maana kumi tofauti kuhusiana na 'udhati wa vitu.'

Mosi, neno 'ni' linamaanisha uwepo wa kitu fulani, mahali fulani, tangu tarehe fulani (being as physical existence).

Mfano, 'Mwezi 'ni' kitu kilicho angani,' Kenya 'ni' Taifa la Afrika,' 'Kilimanjaro 'ni' mlima wa Tanzania,' na 'Nyerere huyu 'ni' mkazi wa Mtwara tangu jana.'

Pili, neno 'ni' linamaanisha 'kitu cha kufikirika' (being as conceptual existence).


Mfano, 'Padre Krismas 'ni' mtu wa kufikirika.' Yaani, 'Padre Krismas 'ni' mtu hewa.'

Tatu, neno 'ni' linamaanisha utambulisho wa kitu kwa njia ya usawa (being as identity). Mfano, 'Nyerere 'ni' Nyerere.' Yaani, 'Nyerere 'ni' sawa na Nyerere' au 'Nyerere 'ni' mtu sawa na Julius.'

Nne, neno 'ni' linamaanisha 'kama' (being as similarity).

Mfano, 'Maudhui ya sanamu ya Julius 'ni' maudhui ya sanamu ya Kenya.' Yaani, 'Sanamu ya Julius 'ni' kama maudhui ya sanamu ya Kenya.'

Tano, neno 'ni' linamaanisha 'kitu



Kamusi

chenye sifa ya' (being as attribution). Mfano, 'mbuzi 'ni' mwekundu.' Yaani 'mbuzi 'ni' kitu chenye sifa ya wekundu.'

Sita, neno 'ni' linamaanisha 'alama ya' (being as signification). Mfano, 'Mkate huu 'ni' mwili wangu,' yaani, 'Mkate huu 'ni' alama ya mwili wangu.'

Saba, neno 'ni' linamaanisha 'mfano wa' (being as instantiation). Mfano, 'Anna 'ni' mtu.' Yaani, 'Anna 'ni' mifano wa mtu katika tabaka la watu.'

Nane, neno 'ni' linamaanisha 'aina ya' (being as typification). Mfano, 'mbuzi 'ni' mamalia.' Yaani 'mbuzi 'ni' aina ya mamalia.'

Tisa, neno 'ni' linamaanisha 'muungano wa' (being as composition). Mfano, 'Tanzania ni Tanganyika na Zanzibar,' yaani 'Tanzania 'ni' muungano wa Tanganyika na Zanzibar.'

Na kumi, neno 'ni' linamaanisha 'finyango la' (being as constitution). Mfano, 'Sanamu ya Nyerere ni dhahabu.' Yaani, 'Sanamu ya Nyerere 'ni' finyango la dhahabu.'

Tukitofautisha maana hizi tutaepuka ulaghai wa kimantiki uitwao 'equivocation,' yaani kutumia neno lenye maana nyingi bila kueleza maana inayokusudiwa.

---

## Utata wa Fumbo la Utatu Mtakatifu

Na Deusedith KAHANGWA

**K**ATIKA Ukristo, Mungu ni mwenye Kakili na utashi, mweza yote, mjua yote, mwenye umilele, mkazi wa mbinguni na duniani, mpenda wote, kaumba vyote, hutawala vyote, na anazo nafsi tatu; yaani Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Fundisho la 'utatu' linayo historia ndefu. Mwaka 325BK, mkutano mkuu wa kwanza wa Nikea ulijadili swali, 'Kuna uhusiano na utofauti gani kati ya Mungu mmoja, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu?'

Mwaka 381, mkutano mkuu wa kwanza wa Konstantinopoli ulijadili swali, 'Roho Mtakatifu ni nafsi ya tatu ya Mungu kweli?'

Mwaka 431, mkutano mkuu wa Efeso ulijadili swali, 'Inawezekanaje Mungu Yesu, ambaye ni muumbaji, kubebwa tumboni mwa Bikra Maria, ambaye ni kiumbe chake?'

Mwaka 451, mkutano mkuu wa Chalisedonia ulijadili swali, 'Ni kweli kwamba Yesu alikuwa na hulka mbili za umungu na ubinadamu, na kama ndio, kivipi?'

Mwaka 553, mkutano mkuu wa pili wa Konstantinopoli ulijadili swali, 'tunawezaje kutafsiri hulka mbili za Yesu mmoja bila kumgawanya mara mbili?'

Mwaka 681, mkutano mkuu wa tatu wa Konstantinopoli ulijadili swali, 'Je, Yesu Kristo alikuwa na vitovu viwili vya maamuzi, kimoja cha kimungu na kingine cha kibinadamu?'

Na mwaka 787, mkutano mkuu wa pili wa Nikea ulijadili swali, 'Je, sanamu za Yesu zinaweza kuabudiwa, na kama ndiyo, kivipi?'

Maazimio ya mikutano hii saba ndio yalizaa fundisho la 'Utatu Mtakatifu.'

Katika kitabu cha Richard Cartwright (1990), 'Philosophical Essays,' kuna andiko, 'On the Logical Problem of the Trinity' limefupisha fundisho hili katika matamko saba, ambayo nimeyapanua na



**Msalaba**

kuzalisha matamko 12 yafuatayo:

(1) Mungu 'ni' Yaweh; (2) Mungu 'ni' nafsi tatu; (3) Baba 'ni' nafsi moja; (4) Mwana 'ni' nafsi moja; (5) Roho Mtakatifu 'ni' nafsi moja; (6) Baba 'ni' Mungu; (7) Mwana 'ni' Mungu; (8) Roho Mtakatifu 'ni' Mungu; (9) Baba 'siyo' Mwana; (10) Mwana 'siyo' Roho Mtakatifu; (11) Roho Mtakatifu 'siyo' Baba; na (12) Mungu 'ni' mmoja tu.

Lakini, neno 'ni' likitafsiriwa kumaanisha utambulisho (identity), basi, kuna mikanganyiko ya kimantiki katika seti hii.

Mfano, matamko namba (6) hadi (8) yanamaanisha kwamba 'Kuna miungu watatu,' wakati tamko namba (12) linasema kuwa 'Mungu 'ni' mmoja tu.'

Na matamko namba (2) hadi (5) yanakanusha matamko namba (6) hadi (8) kwa kumaanisha kwamba Baba siyo Mungu, kwamba Mwana siyo Mungu, na kwamba Roho Mtakatifu siyo Mungu.

Seti yenye mikanganyiko kama hii huwalazimisha waumini kugawanyika kwenye matabaka manne: wanaoikubali, wanaoikosoa, wasiyofungamana na upande, na wanaofungamana na pande zote.

Lakini, binadamu ni kiumbe mwenye urazini unaomtaka kuutafuta ukweli na kuukimbia upotofu. Hivyo, napendekeza tuondoe mikanganyiko kwa kuyahoji na kuyaboresha mapokeo.ends

## Mungu hapendi mikanganyiko

Na Fortunatus BILEGE

**D**AKTARI Dale Tuggy wa Marekani ni mtaalam wa 'falsafa ya uchambuzi wa mambo kwa kutumia kanuni mamboleo za kimantiki,' yaani 'analytical philosophy.'

Ameandika kitabu, 'What is the Trinity?: Thinking about the Father, Son, and Holy Spirit (2017).' Natumia mawazo yake katika hoja yangu ya leo.

Fundisho la 'Utatu Mtakatifu' linaweza kufupishwa katika matamko ya msingi 12 yafuatayo:

(1) Mungu 'ni' Yaweh; (2) Mungu 'ni' nafsi tatu; (3) Mungu Baba 'ni' nafsi moja; (4) Mungu Mwana 'ni' nafsi moja; (5) Mungu Roho Mtakatifu 'ni' nafsi moja; (6) Mungu Baba 'ni' Mungu; (7) Mungu Mwana 'ni' Mungu; (8) Mungu Roho Mtakatifu 'ni' Mungu; (9) Mungu Baba 'siyo' Mungu Mwana; (10) Mungu Mwana 'siyo' Mungu Roho Mtakatifu; (11) Mungu Roho Mtakatifu 'siyo' Mungu Baba; na (12) Mungu 'ni' mmoja tu.

Lakini, matamko haya yanaunda seti yenye utata wa kimantiki. Yaani, matamko namba (2) hadi (5) yanapinga matamko namba (6) hadi (8). Vivyo hivyo, matamko namba (6) hadi (8) yanapinga tamko namba (12).

Kihistoria kuna mikakati mitatu ya kumaliza mikanganyiko hiyo. Mosi, ni kuiondoa kwa kutafsiri upya baadhi ya matamko bila kubadilisha maana yake ya kimapokeo.

Pili, ni kuiondoa kwa kukarabati baadhi ya matamko na hivyo kubadilisha maana yake ya kimapokeo. Na tatu, ni kutumia njia zote mbili.

Mikakati yote hulenga kunyumbulisha neno 'ni' hadi kupata maana inayokubaliana na mapokeo, na inahusisha mbinu kadhaa. Tuone baadhi.

Mbinu ya kwanza, ni kutafsiri neno 'ni' kama ifuatavyo: kwenye tamko namba (1) neno 'ni' linamaanisha 'usawa'; kwenye tamko namba (2) hadi (5) linamaanisha 'kuwa na sifa ya,' ambapo sifa husika ni



*Biblia Takatifu*

'idadi ya nafsi'; kwenye tamko namba (6) hadi (8) linamaanisha 'kuwa na sifa ya umungu'; kwenye tamko namba (9) hadi (11) linamaanisha 'usawa'; na kwenye tamko namba (12) linamaanisha 'kuwa na sifa ya,' ambapo sifa husika ni 'idadi ya miungu.' Hatimaye tunapata fundisho lenye anatomia ifuatayo:

(1') Mungu 'ni sawa na' Yaweh; (2') Mungu 'ana idadi ya' nafsi tatu; (3') Mungu Baba 'ana idadi ya' nafsi moja; (4') Mungu Mwana 'ana idadi ya' nafsi moja; (5') Mungu Roho Mtakatifu 'ana idadi ya' nafsi moja; (6') Mungu Baba 'ana' Umungu; (7') Mungu Mwana 'ana' Umungu; (8') Mungu Roho Mtakatifu 'ana' Umungu; (9') Mungu Baba 'siyo sawa na' Mungu Mwana; (10') Mungu Mwana 'siyo sawa na' Mungu Roho Mtakatifu; (11') Mungu Roho Mtakatifu 'siyo sawa na' Mungu Baba; na (12') Mungu 'ni' mmoja tu kwa idadi.

Mpaka hapo, tumefanikiwa kuondoa ukinzani kati ya tamko namba (6) hadi (8) dhidi ya tamko namba (12). Lakini, bado kuna ukinzani kati ya tamko namba (2) hadi (5) dhidi ya tamko namba (6) hadi (8). Bado tumekwama.

Mbinu ya pili, ni kutafsiri neno 'ni' kama

---

## Mungu hapendi mikanganyiko

*Inatoka Uk. 21*

ilivyofanyika kwenye mbinu ya kwanza, isipokuwa kwenye tamko namba (6) hadi (8), ambapo neno 'ni' linamaanisha 'kuwa sehemu ya.' Hatimaye tunapata fundisho lenye anatomia ifuatayo:

(1<sup>o</sup>) Mungu 'ni sawa na' Yaweh; (2<sup>o</sup>) Mungu 'ana idadi ya' nafsi tatu; (3<sup>o</sup>) Mungu Baba 'ana idadi ya' nafsi moja; (4<sup>o</sup>) Mungu Mwana 'ana idadi ya' nafsi moja; (5<sup>o</sup>) Mungu Roho Mtakatifu 'ana idadi ya' nafsi moja; (6<sup>o</sup>) Mungu Baba 'ni sehemu ya' Mungu; (7<sup>o</sup>) Mungu Mwana 'ni sehemu ya' Mungu; (8<sup>o</sup>) Mungu Roho Mtakatifu 'ni sehemu ya' Mungu; (9<sup>o</sup>) Mungu Baba 'siyo sawa na' Mungu Mwana; (10<sup>o</sup>) Mungu Mwana 'siyo sawa na' Mungu Roho Mtakatifu; (11<sup>o</sup>) Mungu Roho Mtakatifu 'siyo sawa na' Mungu Baba; na (12<sup>o</sup>) Mungu 'ni' mmoja tu kwa idadi.

Mpaka hapo, tumefanikiwa kuondoa ukinzani kati ya tamko namba (6) hadi (8) dhidi ya tamko namba (12). Pia, ukinzani kati ya tamko namba (2) hadi (5) dhidi ya tamko namba (6) hadi (8) umeondoka.

Lakini, kuna changamoto ya kimetafizikia. Mungu kama 'familia' ya nafsi tatu anakuwa ni 'tabaka' au 'seti.'

Lakini, sifa muhimu ya Mungu ni kitovu cha fikra, maamuzi na matendo, yaani ni 'concrete entity.' Hata hivyo, 'tabaka' na 'seti' havina sifa hizo, yaani ni 'abstract entities.' Kwa hiyo, bado tumekwama.

Na mbinu ya tatu, ambalo ni pendekezo langu, ni kutafsiri neno 'ni' kama ilivyofanyika kwenye mbinu ya kwanza, isipokuwa kwa mambo manne.

Kwanza, kwenye kwenye namba (6) neno 'ni' limaanishe 'ni sawa na.' Pili, kwenye tamko namba (7) hadi (8) neno 'ni' limaanishe 'ni kama.'

Tatu, kwenye matamko namba (1), (2), (6), (7), (8) na (12) Mungu anayeongelewa awe ni 'Mungu Mkuu,' yaani 'Godhead.'

Nne, tukiuke mapokeo kwa kusema kuwa, kwenye matamko namba (7) hadi (8), Mwana na Roho Mtakatifu, siyo 'sawa

na Mungu Mkuu,' bali ni 'kama Mungu Mkuu,' jinsi alivyosema Yesu.

Na tano, tukiuke mapokeo tena kwa kusema kuwa, 'Mungu Mkuu' ana 'idadi ya nafsi moja.' Hatimaye tunapata fundisho lenye anatomia ifuatayo:

(1<sup>o</sup>) Mungu Mkuu 'ni sawa na' Yaweh; (2<sup>o</sup>) Mungu Mkuu 'ana idadi ya' nafsi moja; (3<sup>o</sup>) Mungu Baba 'ana idadi ya' nafsi moja; (4<sup>o</sup>) Mungu Mwana 'ana idadi ya' nafsi moja; (5<sup>o</sup>) Mungu Roho Mtakatifu 'ana idadi ya' nafsi moja; (6<sup>o</sup>) Mungu Baba 'ni sawa na' Mungu Mkuu; (7<sup>o</sup>) Mungu Mwana 'ni kama' Mungu Mkuu; (8<sup>o</sup>) Mungu Roho Mtakatifu 'ni kama' Mungu Mkuu; (9<sup>o</sup>) Mungu Baba 'siyo sawa na' Mungu Mwana; (10<sup>o</sup>) Mungu Mwana 'siyo sawa na' Mungu Roho Mtakatifu; (11<sup>o</sup>) Mungu Roho Mtakatifu 'siyo sawa na' Mungu Baba; na (12<sup>o</sup>) Mungu Mkuu 'ni' mmoja tu kwa idadi.

Mpaka hapo, tumefanikiwa kuondoa ukinzani kati ya tamko namba (6) hadi (8) dhidi ya tamko namba (12).

Pia, ukinzani kati ya tamko la (2) hadi (5) dhidi ya tamko la (6) hadi (8) umeondoka. Na sifa ya Mungu kama mtendaji, yaani 'concrete entity' haijaguswa.

Kwa mujibu wa hoja pendekezo langu, Yesu na Roho Mtakatifu 'ni kama' malaika na 'ni kama' Mungu Mkuu. Yaani, wana sifa za 'umungu' zinazowaweka kati ya malaika na Mungu Mkuu.

Kwa kifupi, naona kuwa, pendekezo langu linakubaliana na Biblia, halina mikanganyiko ya kimantiki, linakiuka mapokeo, na linalinda hadhi ya urazini wa kibindamu.

Nihitimishe kwa kusema kuwa, ni uhalifu dhidi ya ubindamu 'kummezsha' mtoto fundisho potofu 'mbili kujumlisha tatu ni saba.'

Na vivyo hivyo, ni uhalifu dhidi ya ubindamu 'kummezsha' mtoto mafundisho ya kidini yaliyojaa upotofu wa kimantiki na kiontolojia. Mungu wetu siyo Mungu wa mikanganyiko.

---



## ‘Red Card’ za Simba mtihani

**T**IMU pinzani zinazocheza na Simba kwa sasa zinapaswa zijiandae kabisa kucheza zikiwa pungufu, kwani rekodi zinaonyesha robo ya mechi za timu hiyo zimesabababishia wapinzani kadi nyekundu.

Ndio, Simba ni timu iliyosababisha kadi nyingi nyekundu kwa wapinzani wake katika mechi inayozihusisha timu hiyo, kwani kati ya kadi 20 zilizoonyeshwa hadi sasa kwenye Ligi Kuu Bara, timu hiyo imehusika na sita, zikiwamo tano zilishowapona wapinzani na moja inayohusu wenyewe.

Rekodi zinaonyesha hadi sasa katika ligi iliyopo raundi ya 20, jumla ya kadi nyekundu 20 zimeonyesha, huku wachezaji wa Polisi Tanzania wakiwa vinara wa kupata kadi nyingi kwani hadi sasa timu hiyo imevuna kadi tano, huku Simba ikiwa kinara dhidi ya wapinzani wake.

Katika mechi iliyofanyika Septemba 14, 2022 kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya, Jamal Masenga wa Prisons alionyeshwa kadi nyekundu dakika ya 90+1 na mwamuzi Ahmed Arajiga baada ya kumkwatua Moses Phiri katika mchezo ambao Simba ilishinda bao 1-0.

Mtibwa Sugar nayo haikupona dhidi ya Simba baada ya wachezaji wake wawili, Pascal Kitenge na Cassian Ponera kuonyeshwa kadi nyekundu katika mchezo uliofanyika Oktoba 30 mwaka jana kwenye uwanja wa Benjamini Mkapa na kumalizika kwa Wekundu wa Msimbazi kushinda mabao 5-0.

Wachezaji hao walionyeshwa kadi nyekundu na mwamuzi Tatu Malogo kwa makosa tofauti, baada ya Kitenge kumuangusha Pape Sakho dakika ya 41 na Ponera dakika ya 67 baada ya kumvuta jezi Augustine Okra wakati akielekea eneo la hatari.

Simba nayo msimu huu hadi sasa imepata kadi nyekundu moja iliyokwenda



*Kocha wa Simba Robertinho Oliveira*

kwa kiungo Sadio Kanoute katika mchezo dhidi ya Coastal Union uliofanyika Uwanja wa Mkwakwani Tanga na kuchezesha na mwamuzi Jonesia Rukyaa na wageni kushinda mabao 3-0.

Timu hiyo pia iliendelea kuwapa umeme wapinzani wao kwani Samson Mbangula wa Prisons naye alilimwa kadi nyekundu na mwamuzi Abdul Wajih baada ya kumfanyia madhambi Henock Inonga dakika ya 20 katika mchezo uliofanyika Desemba 30 Kwa Mkapa na Simba kushinda mabao 7-1.

Pia katika mchezo uliofanyika Januari 18 mwaka huu, Samson Madeleke wa Mbeya City alionyeshwa kadi nyekundu na mwamuzi Ester Adalbert baada ya kumfanyia ‘madhambi’ Sakho.

# POLE SANA RAZA. MOLA AKUAFUU



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Othman Masoud Othman, jana Januari 22, 2023 alimtembelea na kujulia hali Mwakilishi (mstaafu wa Jimbo la Uzini CCM- Unguja), Mohammed Raza Hassanali, nyumbani kwake Mtaa wa Hazrat Abass, Kata ya Kisutu, jijini. Raza anaendelea na matibabu baada ya kupata changamoto ya afya. Kushoto ni mke wa Othman, Zainab Kombo Shaib. Makamu wa Rais aliambatana na Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama hicho na Ismail Jussa Ladhu – hawapo pichani. (Picha kutoka ACT-Wazalendo)

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

